


TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



TAARIFA KWA UMMA

WAOMBAJI WALIODAHILIWA ZAIDI YA CHUO KIMOJA KATIKA AWAMU YA PILI YA UDAHILI, MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inatangaza kuwa udahili kwa awamu ya pili katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2019/2020 umekamilika. Majina ya waombaji waliochaguliwa katika awamu ya pili yameshatangazwa na vyuo husika.

Waombaji waliodahiliwa chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya pili na wale wa awamu ya kwanza ambao bado hawajathibitisha udahili wao katika chuo kimoja, wanasisitizwa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimoja kuanzia tarehe 8 hadi 13 Septemba, 2019. Jinsi ya kujithibitisha ni kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri uliotumwa kupitia namba ya simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyochaguliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kujithibitisha.

Uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti waombaji walizotumia wakati wa kuomba udahili katika vyuo husika. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

Kutokana na baadhi ya waombaji kutochaguliwa katika awamu zilizopita za udahili kwa sababu mbalimbali, Tume inatangaza dirisha la maombi ya udahili awamu ya tatu litafunguliwa kuanzia tarehe **9 hadi 13 Septemba, 2019** ili kuruhusu makundi yafuatayo kuomba udahili:

- Waombaji waliokosa nafasi katika awamu zilizopita;
- Waombaji wa kidato cha sita na stashahada walioshindwa kuomba katika awamu zilizopita; na
- Waombaji waliokuwa wamedahiliwa miaka ya nyuma na kuacha au kukatisha masomo.

Aidha, Tume inapenda kusesitiza kuwa utaratibu wa kutuma maombi ni ule ule wa kutuma maombi moja kwa moja vyuoni kama ilivyokuwa katika awamu za udahili zilizopita. ***Waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili ama kujithibitisha yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika na siyo TCU.***

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa
Katibu Mtendaji
Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania
06 Septemba, 2019